



Aina ya kuunganisha 'splice' na 'cleft'

Baada ya kuunganisha

- Miche inyunyiziwe maji na ikingwe kutokana na wadudu.
- Matawi yote ya mti wa shina (rootstock) yatolewe.
- Boresha miche kwa kuachilia kipindi cha jua pole pole baada ya urefu wa sentimita 10.
- Baada ya mwezi mmoja, uipande mche kwa shamba. Na uondoe karatasi ya kuunganisha.



Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P 57811, NAIROBI.
 Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344
 Barua pepe: resource.centre@kari.org
 Tovuti: www.kari.org

Mtayarishaji:
 Kahinga, J.N.

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

Mkurugenzi wa Kituo,
 KARI-Thika
 S.L.P.220 THIKA

Simu: 067 212281/5, 21134, au 2055038
 Nukulishi: 067 21285
 Barua pepe: karithika@africaonline.co.ke

Vijitabu vya KARI vya taarifa, nambari / 9 / 2008

Shilingi 20 za Kenya

Jinsi ya kuandaa na kuunganisha miche ya matunda ya karakara



Utangulizi

Ukuzaji wa matunda ya karakara husitishwa na wadudu kadhaa na uhaba wa ujuzi kuhusu utanzaji wa mimea miongoni mwa sababu nyingi.

Mkuzaji anastahili kuwa na ujuzi wa kimsingi kuhusu mmea huu.

Sampuli za matunda haya

Aina mbili za matunda ya karakara yanayokuzwa kwa ajili za kuuzwa nchini Kenya.

1) Karakara zambarau (*Passiflora edulis f. edulis*)

Hii huwa ni bora upande wa nyanda za juu kati ya mita 1,100-2,500 juu ya bahari. Mimea hii ina matunda ya rangi ya zambarau ya hali ya juu. Matunda yake huwa na upana wa sentimita 4-5 na ladha yake ni tamu.

Ni mazuri kuuzwa sokoni moja kwa moja au kutengeneza sherbeti ya humu nchini au soko la kimataifa.



Mmea wa karakara zambarau

2) Karakara za manjano (*Passiflora edulis f. flavicarpa*)

Hii huwa ni bora katika sehemu za pwani. Huwa na na tunda lenye upana wa sentimita 5 hadi 7 yenye asidi nyingi na hutumiwa kwa kutengenezea sherbeti. Aina hii huhimili ugonjwa wa *Fusarium wilt*, hata *Phytophthora* na ule wa madoadoa.

Aina hii inatumika kama mti wa mzizi katika kushaliza zambarau ili kuzuia magonjwa ya machanga.



Karakara ya manjano

Kutoa mbegu, kupanda na kuunganisha

Hatua ya kwanza: Kutoa mbegu

Matunda ya manjano yenye kuzaa matunda mengi huchukuliwa:

- Mbegu zinaondolewa kutoka kwa tunda na kuwekwa kwa maji kwa siku 3 ili kuganda na kurahisisha utoaji kutoka kwenye tunda.

- Mbegu zikaushwe chini ya kivuli.

Mbegu zihifadhiwe pahali kavu, baridi na kwenye giza ndiyo zihifadhi ubora wa kuota.

Hatua ya pili: Kupanda

Mbegu zipandwe kwenye vitalu vilivyotayarishwa vya sentimita 6 kwa 22.5 au katika mifuko ya plastiki iliyojazwa mchanga safi kuzuia minyoo ya mizizi (*root knot nematodes*), magonjwa ya mchanga, au viumbe hai vinginevyo vyenye madhara.

- Miale ya jua au mvuke wa maji zaweza kutumiwa kuondoa madhara ya mchanga.
- Mbegu huota baada ya siku 17.

Hatua ya tatu: Kupandilia

Miche ikuzwe hadi iwe ya sentimita 50 na 3 hadi 4 kwa upana.

- Miche yenye afya na rangi ya kijani kibichi kilichokolea itumiwe kupandilia.
- Sehemu za miche ya matunda ya zambarau yakatwe hasa baada ya mmea kuwa na maua.

Miche hiyo ipandwe mahali hamna wadudu au magonjwa.

- Usafi wa vyombo vya kukata kati ya kukata mmea moja na mwingine sharti ufanywe kwa kuitumia JIK.
- Aina mbili za kuunganisha zinatumiwa ambazo ni 'cleft' na 'splice'.